JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

## IDARA YA MISITU NA NYUKI

# MWONGOZO RAHISI WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA PAMOJA

**Kwa Ajili ya Ushirikishwaji wa Jamii katika Usimamizi wa Misitu ya Hifadhi**

Umetayarishwa na Kampeni ya Mama Misitu kwa niaba ya Idara ya Misitu na Nyuki

Dar es Salaam
**Oktoba, 2015**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

## IDARA YA MISITU NA NYUKI

# MWONGOZO RAHISI WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA PAMOJA

**Kwa Ajili ya Ushirikishwaji wa Jamii katika Usimamizi wa Misitu ya Hifadhi**

Umetayarishwa na Kampeni ya Mama Misitu kwa niaba ya Idara ya Misitu na Nyuki

Dar es Salaam
**Oktoba, 2015**

## UTANGULIZI

Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002 inabainisha wazi katika vifungu vya 34, 35 na 36 kuwa Mkurugenzi wa Misitu atatoa miongozo, au “maelezo ya maelekezo” kuhusu usimamizi wa Misitu ya Hifadhi, ambayo mameneja wa msitu watalazimika kuizingatia.

Mwaka 2007, Idara ya Misitu na Nyuki (IMN) ilichapisha toleo la kwanza la mwongozo wa kuwezesha Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja (USMP) – kwa nia ya kuwezesha jamii kushiriki katika usimamizi wa Misitu ya Hifadhi ya Serikali.

Mwaka 2013 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, mwongozo huo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja ulipitiwa ili kukidhi mahitaji ya wadau hao hususan katika eneo la utaratibu wa mgawanyo wa majukumu na mafao baina ya washiriki katika mkataba wa usimamizi. Mwongozo huu ulitolewa kwa lugha ya kiingereza ambayo siyo rafiki kwa watumiaji wengi na jamii kwa ujumla.

Kuna haja kubwa ya kuitika kilio cha wadau kwa kutafsiri mwongozo huu katika lugha ya Kiswahili  ili kukidhi mahitaji ya wadau na jamii na hivyo kuwezesha kusukuma mbele juhudi za ushiriki wa jamii katika kusimamia rasilimali hii muhimu ya misitu.


Kijitabu hiki kimeandikwa kwa ajili ya wataalam wa misitu wanaofanyakazi ya kuwezesha Usimamizi wa Misitu ya Serikali kwa kushirikisha jamii zinazopakana nayo, Asasi zisizokuwa za Kiserikali na sekta binafsi. Kijitabu hiki kinatoa mwongozo rahisi wa kuwezesha jamii na wadau wote kushiriki katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja katika maeneo yao.

Idara ya Misitu na Nyuki inatoa shukrani kwa wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika uandaaji na uboreshaji wa tafsiri hii rahisi. Kipekee, tunatoa shukrani kwa Kampeni ya Mama Misitu kwa kuwezesha utengenezaji na uchapishaji wa kijitabu hiki.

Gladness A. Mkamba
Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Misitu na Nyuki,
Wizara ya Maliasili na Utalii
2015

## MUHTASARI

Misitu yetu inakabiliwa na tishio la kutoweka. Usimamizi Shirikishi wa Misitu ni mojawapo ya mikakati Serikali ya kuweka misitu mingi iwezekanavyo chini ya usimamizi madhubuti na endelevu. Hii imewekwa dhahiri katika Sera ya Taifa ya Misitu na Sheria ya Misitu.




Mwongozo huu una sehemu kuu nne:

**Sehemu ya I: Utangulizi**

Sehemu hii hutoa maelezo ya utangulizi kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja.

**Sehemu ya II: Misingi ya kisheria ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja**

Sehemu hii inabainisha baadhi ya vipengele muhimu vya kisheria vya Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamojandani ya Sheria ya Misitu na Sheria ya Serikali za Mitaa

**Sehemu ya III: Mchakato wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja**

Sehemu hii inaainisha mchakato pendekezwa katika kuweka misitu chini ya usimamizi Shirikishi wa Pamoja.

**Sehemu ya IV: Sanduku la msaada la Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja**

Sehemu hii inatoa mifano rahisi ya baadhi ya zana za kufanya tathmini ya rasilimali za msitu, kurasa za mfano za kumbukumbu muhimu za kutunzwa na mameneja wa misitu, pamoja na muundo sampuli unaotumika kwenye Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja (sheria ndogo, Mpango wa Usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji na Makubaliano/mkataba wa Usimamizi wa Pamoja). Siyo lazima kufuata miundo hii: inatolewa kukupa mwongozo tu.

**Tumerithi. Tuwarithishe!**

SEHEMU YA I

# UTANGULIZI

## Nini maana ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja na ni kwa jinsi gani unatofautiana na Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii?

Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) ni neno la ujumla linaloelezea ushiriki wa jamii katika usimamizi wa misitu. Kuna aina mbili za mbinu za Usimamizi Shirikishi wa Misitu :

**Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja** ni mbinu shirikishi ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu  ambayo hufanyika katika misitu iliyopo kwenye"Ardhi ya Hifadhi" –ardhi ambayo tayari imeshatengwa (ama imehifadhiwa) na mamlaka za kiserikali. Msitu unasimamiwa kwa pamoja kati ya mmiliki na wadau mbalimbali, kama vile jamii, sekta binafsi, serikali za mitaa au serikali kuu au mtu mwingine aliyeidhinishwa na Idara ya Misitu na Nyuki. Hitimisho la mchakato huu ni Mkataba wa kisheria wa Usimamizi wa Pamoja unaoelezea jinsi gharama na faida za usimamizi wa misitu kwa pamoja zitakavyogawanywa baina ya mmiliki wa msitu na msimamizi mwenza, yaani vijiji vya jirani vinavyoshiriki katika usimamizi.

**Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii** ni aina ya pili ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ambayo hufanyika katika ardhi ya kijiji, katika misitu inayomilikiwa na kusimamiwa na Halmashauri ya Kijiji kwa niaba ya Kijiji na kupelekea uanzishwaji wa Misitu ya Hifadhi ya Kijiji, Misitu ya hifadhi ya Jamii au Misitu ya Hifadhi Binafsi.

Mwongozo huu unahusu **Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja tu.**

**Misingi Minane Muhimu kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja**

**1. Jamii kama wasimamizi/mameneja wa msitu**


Usimamizi shirikishi wa misitu kwa pamoja unahamasisha jamii zinazopakana na msitu kuwajibika katika usimamizi wa msitu kwa kulinda msitu na kufanya doria. Kutokana na majukumu haya jamii inastahili kupata mafao kama haki za kuvuna mazao ya misitu, kupata gawio la maduhuli kutokana na mavuno ya mazao ya misitu, kubakiza fedha zitokanazo na faini na mazao yaliyotaifishwa, kutumia vyanzo vya maji n.k.

**2. Usimamizi Shirikishi wa Misitu unavyoweza kutumika katika Aina zote za Misitu**

Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii unaweza kufanyika katika aina zote za msitu - yenye bioanuwai nyingi au chache, iliyofunga au iliyoharibiwa, mikubwa au midogo, misitu ya milimani, matajiwazi au mikoko, misitu ya kupandwa au ya asili. Malengo ya mfumo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja yanaweza kuwa ni uhifadhi au uzalishaji au mchanganyiko wa yote. Jambo la msingi kuelewa ni kwamba Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja hufanyika kwenye misitu inayomilikiwa na mdau mmoja (kwa kawaida huwa ni Serikali) na usimamizi unafanyika kwa kushirikisha wadau wengine.

**3. Jamii kama Walengwa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja**

Wanakijiji au jamii kwa muktadha huu inamaanisha watu wale wanaoishi msituni au jirani na msitu na ni kundi lengwa la Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja kutokana na uhusiano wao wa kihistoria na ukaribu wao na msitu unaowafanya kuwa na uwezo wa kusimamia msitu kwa madhubuti na uendelevu.



**4. Jamii kama watoa maamuzi na siyo walinzi tu**

'Usimamizi' katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja unahusisha mambo yote ya usimamizi wa misitu, kama vile ulinzi wa misitu, udhibiti wa

upatikanaji na matumizi ya mazao ya misitu, na shughuli za uboreshaji au kuongeza uwezo wa upatikanaji wa mazao ya misitu. Unajumuisha sio tu wajibu wa usimamizi kivitendo bali pia mamlaka ya kufanya maamuzi, yanayoongoza shughuli hizo.




### 5. Usawa katika mgawanyo wa gharama na mafao ya usimamizi wa misitu

Kwa kuwa kuna pande mbili zinazohusika katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja, ni muhimu sana kuwapo kwa makubaliano dhahiri kuhusu jinsi majukumu ya usimamizi yatakavyogawanywa. Hii itaondoa migongano wakati usimamizi utakapoanza. Pia ni muhimu kubainisha mafao yatokanayo na usimamizi wa msitu na kukubaliana wakati wa majadiliano. Ni muhimu kuweka ulinganifu/uwiano kati ya gharama za jamii katika usimamizi wa misitu na faida watakazopata. Kutokuwa na makubaliano yenye usawa kutaathiri uendelevu wa makubaliano katika siku za usoni na hivyo kutochangia kwenye lengo la kupunguza umaskini.


### 6. Kutumia kikamilifu Mfumo uliopo kijijini

Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja hauanzishi taasisi mpya bali unatumia taasisi zilizopo. Unatumia mfumo wa vijiji kwenye Halmashauri za Vijiji ambazo zina dhima na mamlaka yanayoweza kutumika vizuri katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii. Hii ni pamoja na haki ya kutunga sheria ndogo za kijiji, zinazowezesha kanuni za jamii kupewa uzito unaostahili wa sheria halali. Kisheria, halmashauri za Vijiji zinatenda kazi kwa niaba ya wanakijiji na zinawajibika kwao.

**7. Kubadilika kwa jukumu la idara ya misitu na wataalam wa halmashauri za wilaya**

Hapo zamani watumishi wa serikali katika sekta ya misitu walitekeleza majukumu yao kama polisi - kuzuia jamii kujihusisha na matumizi na usimamizi ya misitu. Chini ya Sheria mpya ya Misitu, majukumu mapya ya wataalamu wa misitu wa Wilaya ni kuwasaidia wanakijiji kutambua, kupima misitu, na kusimamia misitu yao wenyewe kwa manufaa ya jamii nzima. Kwa sasa, wataalamu wa misitu wa serikali wanafanya kazi kama washirika wa jamii, wakiwashauri jinsi gani wanaweza kusimamia misitu yao kwa ubora zaidi na kwa malengo ya muda mfupi na muda mrefu.

Katika mchakato huu uhusiano wa wataalam na jamii unabadilika, kutoka jukumu la kipolisi na kuwa:




**8. Mwongozo Sio Amri**

Mwongozo huu unatoa maelezo kuhusu mahitaji ya kisheria katika kujadiliana kuhusu Makubaliano ya Usimamizi wa Pamoja, kwa hiyo unapaswa kufuatwa. Sehemu ya III inatoa maelezo ya kila hatua inayotakiwa katika kuwezesha Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja. Kama ukiona kwamba una njia nyingine rahisi ya kufikia mahitaji haya ya kisheria, basi si lazima kufuata hatua za mwongozo huu jinsi zilivyo.

# MISINGI YA KISHERIA YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA PAMOJA

## Nani anaweza kutekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja?

Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja unahalalishwa kisheria kwa kusaini Makubaliano /mkataba wa Usimamizi kwa Pamoja (MUP).

Makubaliano /mkataba wa Usimamizi kwa Pamoja unaweza kufanywa kati ya:

- Idara ya Misitu na Nyuki/Wakala wa Huduma za Misitu na mtu ye yote au taasisi ya kijamii au sekta binafsi kusimamia Msitu wa Hifadhi wa Taifa;
- Idara ya Misitu na Nyuki/Wakala wa Huduma za Misitu na makundi ya jamii au makundi ya watu wanaoishi jirani na wanaojipatia mahitaji yao yote au sehemu ya maisha yao kutoka kwenye Msitu wa Hifadhi wa Taifa;
- Halmashauri ya wilaya, halmashauri ya kijiji, kikundi cha jamii au mtu ye yote au taasisi ya jamii au sekta binafsi kusimamia Msitu wa Hifadhi wa Tawala ya Mitaa;
- Meneja wa msitu binafsi na makundi ya jamii au makundi ya watu wanaoishi jirani na wanaojipatia mahitaji yao yote au sehemu ya maisha yao kutoka kwenye au jirani na msitu binafsi.

Halmashauri za vijiji zinaweza kuwasilisha maombi ya kusimamia kwa pamoja sehemu au Msitu wote wa Hifadhi kwa Mkurugenzi wa Misitu/ Mtendaji mkuu wa Wakala wa Huduma za misitu (kama ni Msitu wa Hifadhi wa Taifa) au Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kama ni Msitu wa Hifadhi wa serikali za Mtaa. Sheria ya Misitu: Eneo ndani ya Msitu wa Hifadhi linalosimamiwa na kijiji linaitwa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji.

Serikali za Vijiji, ASASI zisizokuwa za kiserikali, kampuni yenye mkataba wa msitu au kikundi cha jamii kinaweza kuwa meneja mteule kusimamia msitu wa serikali. Mamlaka kamili ya usimamizi (yaani gharama za usimamizi na mafao) vinahamishwa kutoka meneja mmoja kwenda kwa mwingine. Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki baada ya kujadiliana na Waziri kupitia Kamati ya Ushauri wa Misitu ya Taifa anaweza kuhamisha mamlaka ya usimamizi kutoka Serikali Kuu au Halmashauri ya Wilaya kwenda upande mwingine.

## Ni mahitaji gani ya kisheria yanatakiwa ili kuanzisha Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja?

**1. Kuchagua Kamati ya kijiji ya Usimamizi wa Maliasili**

Kamati ya Maliasili ya Kijiji lazima ichaguliwe na Mkutano Mkuu wa Kijiji na si kuteuliwa na Halmashauri ya Kijiji na ni lazima izingatie masuala ya jinsia. Kwa mujibu wa sheria, kamati hii ndio chombo kikuu kinachohusika na usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji

**2. Kubainisha mipaka ya nje na ya ndani ya misitu**

Sheria inataka mipaka ya kila msitu wa hifadhi iweze kuwekwa alama. Kama msitu unapakana na vijiji zaidi ya kimoja, vijiji shiriki vinaweza kuamua kugawana usimamizi wa msitu katika maeneo tofauti ya usimamizi kwa kila kijiji. Maeneo haya huitwa 'Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji. Hata hivyo, vijiji vinaweza kuamua kusimamia msitu wote bila kuugawanya katika maeneo ya usimamizi ya vijiji

**3. Kuandaa mpango wa usimamizi wa msitu**

Afisa Misitu kwa kushirikiana na vijiji vinavyopakana na msitu kuandaa mpango wa usimamizi wa msitu wote kwa kuzingatia malengo makuu ya msitu husika (Uhifadhi au Matumizi). Kama msitu ni wa matumizi, Mpango wa usimamizi uweke bayana viwango vya uvunaji na matumizi. Kama jamii zitaamua kusimamia kipekee maeneo ya usimamizi wa misitu ya vijiji, inashauriwa kuwa mipango ya eneo la usimamizi wa msitu la kijiji iandaliwe kwa kila kijiji.

**4. Kuandaa Makubaliano/mkataba wa usimamizi wa pamoja.**

Mkataba unatiwa saini baina ya mmiliki wa msitu (Serikali kuu au Serikali ya Mtaa) na serikali za vijiji vinavyopakana na msitu vinavyoshiriki kusimamia msitu. Mkataba unaweza kutiwa saini na kila kijiji (mikataba mingi) kwa ajili ya usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji au na vijiji vyote katika mkataba mmoja.

Taarifa muhimu zinazopaswa kuwa ndani ya Makubaliano/Mkataba wa Usimamizi wa Pamoja:

- Jina la maelezo ya msitu
- Maelezo ya mambo yaliyokubaliwa (mf. Kijiji X kitasimamia Eneo la Usimamizi wa msitu la kijiji X)
- Madhumuni ya makubaliano/mkataba
- Wanaoingia makubaliano/mkataba
- Jinsi majukumu ya usimamizi yatakavyo gawanywa
- Kanuni zitakazotumika
- Jinsi mapato yatokanayo na usimamizi wa msitu (faini, tozo)

yatakavyosimamiwa na kutumika

- Taratibu za kutatua migogoro inayoweza kujitokeza miongoni mwa wadau kati makubaliano/mkataba
- Kipindi/muda wa makubaliano/mkataba
- Jinsi mkataba unavyoweza kurejewa.

**5. Kuandaa sheria ndogo za kijiji za usimamizi shirikishi wa misitu kwa pamoja**

Ili kuwezesha wanakijiji kutekeleza makubaliano ngazi ya kijiji (ikihusisha kutoza faini na kukamata wahalifu), kijiji kinapaswa kuandaa sheria ndogo za vijiji na kuhakikisha zinaidhinishwa na Baraza la madiwani la Halmashauri ya wilaya. Kama msitu utasimamiwa kwa pamoja na vijiji vyote bila kugawana maeneo, sheria ndogo zifanane kwa kila kijiji. Hata hivyo, zitapaswa kuidhinishwa na kila mkutano mkuu wa kila kijiji.

**Jinsi majukumu na mafao yanavyogawanywa katika Usimamzi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja**

Malipo ya maduhuli yatokanayo na uvunaji wa mazao ya misitu, ushuru na ada zingine kulipwa kwa utaratibu ufuatao:

- Sehemu moja ya malipo ifanywe kwa mmiliki wa msitu (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS au Halmashauri ya Wilaya).
- Sehemu ya pili (ushuru wa usimamizi wa jamii) ulipwe kwenye akaunti ya kijiji (kijiji ambako miti imevunwa kutoka kwenye eneo la usimamizi wa msitu la kijiji).

**Masharti ya jamii kupata mafao**

Vijiji vitastahili kupokea mapato pale tu:

- Vitakaposaini mkataba wa makubaliano ya usimamizi kati yao na mmiliki wa msitu (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS au Halmashauri ya Wilaya)
- Vitakapotekeleza majukumu yaliyoainishwa kwenye mkataba wa makubaliano ya usimamizi.

## MCHAKATO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA PAMOJA

### HATUA YA KWANZA: NAMNA YA KUANZA

**Shughuli Muhimu Ngazi ya Wilaya**

1. Chagua msitu wa kuanza mchakato wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja kutokana na umuhimu wa msitu husika
2. Bainisha wajibu na majukumu na anzisha mahusiano na maafisa misitu na watumishi wengine wa serikali:

Kwa msitu wa hifadhi wa taifa, utakuwa chini ya mamlaka ya Meneja wa Misitu wa Wilaya. huyu ndiye ataongoza mchakato wa kuanzisha Usimamizi Shirikishi wa Msitu kwa Pamoja akishirikiana na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya. Kwa msitu wa hifadhi wa Mamlaka ya Serikali za Mtaa mchakato utaongozwa na Halmashauri ya Wilaya na kushirikisha watumishi wa wakala wa huduma za misitu kama wapo.

**Shughuli Muhimu Ngazi Ya Kijiji**

1. Kutana na Serikali ya Kijiji na kutambulisha dhana na misingi ya Usimamizi Shirikishi Wa Misitu kwa Pamojana na elezea mchakato wa namna ya kupanga.




2. Kutana na kijiji kizima kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji na elezea malengo na madhumuni ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja na mahitaji ya kupanga Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja. Kijiji kichague wajumbe wa Kamati ya Maliasili wakati huu.




3. Kutana na timu ya kamati ya maliasili ya Kijiji na kubaliana wakati wa kuanza, wakati gani na wapi pa kukutana. Waelezee hatua za Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamojana ni muda gani mchakato unaweza kuchukua.

## HATUA YA PILI: TATHMINI NA MPANGO WA USIMAMIZI

***Shughuli Muhimu ni Pamoja na***

1. Tambua na zungukia mipaka yote ya kijiji pamoja na wajumbe wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji na viongozi wengine wa kijiji. Alama zote za mipaka zirekodiwe (mf: mito, barabara kubwa, miamba, miti mikubwa).

2. Kama msitu unapakana na vijiji zaidi ya kimoja, unaweza kugawanywa katika maeneo tofauti ya usimamizi kwa kila kijiji linaloitwa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji.

   Pamoja na wajumbe wa kamati za Maliasili tembea msituni na baini mipaka ya kila Eneo la Usimamizi la Msitu la Kijiji. Mipaka hii inaweza kuwa ni mito, vijito, barabara, vilele vya vilima na mabonde. Hakikisha Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji linawekwa bayana kwenye ramani na kuthibitishwa kwa GPS.




3. Soma mpango wote wa usimamizi wa msitu uliopo kwa kushirikiana na timu ya uwezeshaji. Mpango wa usimamizi wa msitu uliopo kujadiriwa na wadau wote na kuwasilishwa kwenye vijiji vyote vilivyotayari kushiriki kusimamia msitu ili kutambua fursa zilizopo na mafao yaliyopo.

4. Fanya tathmini shirikishi ya rasilimali za msitu kwa kushirikiana na Kamati ya Maliasili ya Kijiji ili kubaini matumizi ya misitu na watumiaji, kutenga eneo la msitu katika "Kanda za Usimamizi wa Msitu" kwa kuzingatia mapendekezo ya malengo ya usimamizi, kufanya tathmini ya miti na msitu ndani ya kila kanda, kuchambua matokeo na kuwasilisha matokeo kwenye mkutano mkuu wa kijiji kwa ajili ya majadiliano na kibali.

5. Wasilisha na afikiana kuhusu mgawanyo wa majukumu na mafao yatokanayo na Usimamizi Shirikishi wa Msitu kwa Pamoja.

**Mgawanyo wa majukumu na mafao katika Usimamizi Shirikishi wa Msitu kwa Pamoja**

Majedwali manne yanayotoa mwongozo wa majukumu ambayo jamii zitapaswa kutekeleza ili ziweze kustahili kupata mafao yamebainishwa kama ifuatavyo:

**Misitu ya hifadhi (Vyanzo vya maji)**

| Majukumu ya Jamii (Masharti ya Kupata Mafao) | Mafao kwa Jamii (Masharti baada ya kutimiza majukumu) |
|---|---|
| Kushiriki katika kuandaa na kutekeleza makubaliano ya usimamizi wa msitu wa pamoja | Asilimia 44 ya faida itokanayo na mauzo ya kaboni italipwa kwa jamii na kiasi kilichobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |

| | |
|---|---|
| Kufanya doria na kutekeleza sheria zilizoainishwa kwenye mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu | Asilimia 32 ya faini kwa uhalifu uliofanyika kwenye eneo la usimamizi la kijiji itabaki kijijini na kiasi kilichobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |
| Kuzuia, kudhibiti na kuzima moto kwenye eneo la Usimamizi wa Msitu la kijiji | Asilimia 35 ya ushuru wa vibali vya utafiti, kuingia, kuweka kambi, minara ya mawasiliano na kupiga picha italipwa kwa serikali ya kijiji na inayobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu. |
| Kufanya Mikutano ya vijiji kila baada ya miezi mitatuna kamati ya maliasili ya kijiji kila mwezi kujadili masuala ya usimamizi wa msitu | Asilimia 25 ya maduhuli yatokanayo na utalii wa ikolojia yatalipwa kwa jamii na kiasi kilichobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |
| Kudhibiti vitendo vya uhalifu na kutoa taarifa kwa wakati kwa ngazi na mamlaka zinazo husika | Asilimia 49 ya maduhuli halisi kutokana na mazao ya misitu yaliyotaifishwa yaende kwa serikali ya kijiji na nyingine 51% iende kwenye mfuko wa misitu/ halmashauri ya Wilaya. Vifaa na zana zilizotaifishwa zitachukuliwa na mmiliki wa msitu wa hifadhi. |
| Kudhibiti wanyama waharibifu na upotevu wa mazao, mali na maisha ya watu kwa kushirikiana na mmiliki wa msitu | Fursa za ajira katika shughuli mbalimbali za usimamizi wa msitu |
| Kuimarisha maeneo ya utalii na kuhakikisha usalama wa watalii, wanafunzi na watafiti kwenye maeneo ya usimamizi | Matumizi ya miti ya mbao iliyoanguka nje ya ukanda wa hifadhi kwa kibali |

| | |
|---|---|
| Kuondoa mimea vamizi (kwa kuzingatia tafiti na usimamizi) na kuziba mapengo kwa kupanda aina za miti (spishi) sahihi kwa eneo husika na kuruhusu uoto wa asili ili kuhakikisha uboreshaji wa bioanuwai | Kuingia msituni kukusanya mboga za majani, uyoga, kuchukua dawa bila kuathiri mti, kuokota mbegu, kamba, kukata nyasi kwa ajili ya malisho na kuezekea, kuni kavu na kuokota matunda. Pia kupita njia za miguu kutoka Kijiji kimoja hadi kingine, kuhudumia maeneo ya makaburi, kugema ulanzi, kufanya matambiko na kuchota maji kwa matumizi ya nyumbani na kilimo kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira |
| Kutoa taarifa ya utekelezaji na ufuatiliaji kwa maandishi ya kila robo mwaka kwa mmiliki wa msitu | Kuingia msituni kwa shughuli za ufugaji Nyuki kitaalam kwa kibali |
| Halmashauri ya kijiji kutoa taarifa ya mapato na matumizi katika mikutano mikuu ya Kijiji kila robo mwaka | Kuingia msituni kwa shughuli za uvuvi na uwindaji utafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni za sekta husika |
| Kamati ya maliasili ya kijiji kuandaa na kutunza kumbukumbu sahihi za usimamizi wa msitu. | |
| Kushiriki katika kuzuia na kudhibiti shughuli za uharibifu katika vyanzo vya maji na mazingira ndani na nje ya misitu katika vijiji husika. | |
| Kushiriki katika mikutano yote inayohusu usimamizi shirikishi wa misitu ya hifadhi | |
| Kuhakikisha kuwa alama za mipaka ya misitu haziharibiwi wala kuhamishwa | |

**Misitu ya hifadhi (Mazingira Asilia)**

| Majukumu ya Jamii (Masharti ya Kupata Mafao) | Mafao kwa Jamii (Masharti baada ya kutimiza majukumu) |
|---|---|
| Kushiriki kuandaa na kutekeleza makubaliano ya usimamizi wa msitu | Asilimia 46 ya faida itokanayo na uuzaji wa hewa ukaa italipwa kwa jamii na kiasi kilichobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |
| Kufanya doria na utekelezaji wa sheria zilizoainishwa kwenye mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu wa Pamoja | Asilimia 32ya faini kwa uhalifu uliofanyika kwenye eneo la usimamizi la kijiji itabaki kijijini na kiasi kilichobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |
| Kuzuia, kudhibiti na kuzima moto kwenye eneo la Usimamizi wa Msitu | Asilimia 36 ya ushuru wa vibali vya utafiti, kuingia, kuweka kambi, minara ya mawasiliano na kupiga picha italipwa kwa serikali ya kijiji na inayobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu. |
| Kufanya Mikutano ya vijiji kila baada ya miezi mitatu na kamati ya maliasili ya kijiji kila mwezi kujadili masuala ya usimamizi wa msitu | Asilimia 26 ya maduhuli yatokanayo na utalii ikolojia yatalipwa kwa jamii na kiasi kilichobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |
| Kudhibiti vitendo vya uhalifu na kutoa taarifa sahihi ya maandishi na kwa wakati kwa ngazi na mamlaka zinazo husika | Asilimia 49 ya maduhuli halisi kutokana na mazao yaliyotaifishwa yaende kwa serikali ya kijiji na nyingine iende kwenye mfuko wa misitu/halmashauri ya Wilaya. Vifaa na zana zilizotaifishwa zitachukuliwa na mmiliki wa msitu. |
| Kudhibiti wanyama waharibifu na upotevu wa mazao, mali na maisha ya watu kwa kushirikiana na mamlaka husika | Fursa ya ajira katika shughuli mbalimbali za usimamizi wa msitu |
| Kuimarisha maeneo ya utalii na kuhakikisha usalama wa watalii, wanafunzi na watafiti kwenye maeneo ya usimamizi | |

| | |
|---|---|
| Kuondoa mimea vamizi (kwa kuzingatia tafiti na usimamizi) na kuziba mapengo kwa kupanda aina za miti (spishi) sahihi kwa eneo husika na kuruhusu uoto wa asili ili kuhakikisha uboreshaji wa bioanuwai | Kuingia msituni kuchuma mboga za majani, uyoga, kuchukua dawa bila kuathiri mti, kuokota mbegu, kamba, kukata nyasi kwa ajili ya malisho na kuezekea, kuni kavu na kuokota matunda. Pia kupita njia za miguu kutoka Kijiji kimoja hadi kingine, kuhudumia maeneo ya makaburi, kugema ulanzi, kufanya matambiko na kuchota maji kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira |
| Kutoa taarifa ya utekelezaji na ufuatiliaji kwa maandishi ya kila mwezi kwa mmiliki wa msitu | Kuingia msituni kwa shughuli za ufugaji Nyuki |
| Kutoa taarifa ya mapato na matumizi katika mikutano mikuu ya Kijiji kila robo mwaka | Kupata maji safi na salama kwa matumizi ya nyumbani na kilimo nje ya hifadhi |
| Kuandaa na kutunza kumbukumbu sahihi za usimamizi wa msitu. | |
| Kushiriki katika kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira ndani na nje ya misitu katika vijiji husika. | |
| Kushiriki katika mikutano yote inayohusu usimamizi shirikishi wa misitu ya hifadhi | |
| Kuhakikisha kuwa alama za mipaka ya misitu haziharibiwi wala kuhamishwa | |

**Misitu ya hifadhi (Matumizi)**

| Majukumu ya Jamii (Masharti ya Kupata Mafao) | Mafao kwa Jamii (Masharti baada ya kutimiza majukumu) |
|---|---|
| Kushiriki katikaKuandaa na kutekeleza makubaliano ya usimamizi wa msitu | Asilimia 41 ya faida itokanayo na uuzaji wa hewa ukaa italipwa kwa jamii na kiasi kilichobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |
| Kufanya doria na utekelezaji wa sheria zilizoainishwa kwenye mpango wa Usimamizi wa Shirikishi wa Misitu wa Pamoja | Asilimia 32ya faini kwa uhalifu uliofanyika kwenye eneo la usimamizi la kijiji itabaki kijijini na kiasi kilichobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |
| Upandaji miti msituni kuziba mapengo kwa kutumia aina za miti (spishi) sahihi | Asilimia19 ya mrabaha utokanao na mauzo ya mazao ya misitukulipwa kwa serikali ya kijiji na kiasi kilichobaki kulipwa kwa mmiliki wa msitu wa Hifadhi |
| Kufanya Mikutano ya vijiji kila baada ya miezi mitatu na kamati ya maliasili ya kijiji kila mwezi kujadili masuala ya usimamizi wa msitu | Asilimia 46 ya maduhuli halisi kutokana na mazao yaliyotaifishwa yaende kwa serikali ya kijiji na nyingine iende kwenye mfuko wa misitu/halmashauri ya Wilaya. Vifaa na zana zilizotaifishwa zitachukuliwa na mmiliki wa msitu. |
| Kutoa taarifa ya utekelezaji na ufuatiliaji kwa maandishi ya kila mwezi kwa mmiliki wa msitu | Fursa ya ajira katika shughuli mbalimbali za usimamizi wa msitu |
| Kudhibiti na kuzima moto kwenye eneo la Usimamizi wa Msitu | Kuingia msituni kwa shughuli za ufugaji Nyuki |
| Kusimamia shughuli za uvunaji ikiwa ni pamoja na kushiriki kuainisha maeneoya uvunaji na kufanya tathmini ya rasilimali za misitu | Kuingia msituni kuchuma mboga za majani, uyoga, kuchukua dawa bila kuathiri mti, kuokota mbegu, kamba, kukata nyasi kwa ajili ya malisho na kuezekea, kuni kavu na kuokota matunda. Pia kupita njia za miguu kutoka Kijiji kimoja hadi kingine, kuhudumia maeneo ya makaburi, kugema ulanzi, kufanya matambiko na kuchota maji kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira |

| | |
|---|---|
| Kuwa na vitalu vya miti na kuipanda miti katika mashamba yao | Kuingia msituni kwa shuguli za uvuvi na uwindaji kutafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni za sekta husika |
| Kutoa taarifa ya mapato na matumizi katika mikutano mikuu ya Kijiji kila robo mwaka | Asilimia 35 ya ushuru wa vibali vya utafiti, kuingia, kuweka kambi, minara ya mawasiliano na kupiga picha italipwa kwa serikali ya kijiji na inayobaki kwenda kwa mmiliki wa msitu. |
| Kuandaa na kutunza kumbukumbu sahihi za usimamizi wa msitu. | |
| Kushiriki katika kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira ndani na nje ya misitu katika vijiji husika. | |
| Kushiriki katika mikutano yote inayohusu usimamizi shirikishi wa misitu ya hifadhi | |
| Kuhakikisha kuwa alama za mipaka ya misitu haziharibiwi wala kuhamishwa | |

**Mashamba ya miti**

| Majukumu ya Jamii (Masharti ya Kupata Mafao) | Mafao kwa Jamii (Masharti baada ya kutimiza majukumu) |
|---|---|
| Kushiriki katikaKuandaa na kutekeleza makubaliano ya usimamizi wa msitu | Asilimia 27 ya faida itokanayo na miradi ya CDM (Clean Development Mechanism) zitalipwa kwa jamiina faida inayobaki itaenda kwa mmiliki wa shamba la miti |
| Kufanya doria na kutekeleza sheria, zilizoanishwa kwenye mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja | Asilimia 46 ya maduhuli halisi kutokana na mazao yaliyotaifishwa yaende kwa serikali ya kijiji na nyingine iende kwenye mfuko wa misitu/halmashauri ya Wilaya. Vifaa na zana zilizotaifishwa zitachukuliwa na mmiliki wa shamba la miti. |

| | |
|---|---|
| Kutoa nguvukazi kwa kazi mbalimbali za misitu zitakazotakiwa kutekelezwa | Asilimia 36 ya ushuru wa vibali vya utafiti, kuingia, kuweka kambi, minara ya mawasiliano na kupiga picha italipwa kwa serikali ya kijiji na inayobaki kwenda kwa mmiliki wa shamba la miti. |
| Kushiriki kikamilifu na kwa uwazi kusimamia shughuli za uvunaji wa mazao ya misitu na Nyuki. | Asilimia 32 ya faini kwa uhalifu uliofanyika kwenye eneo la usimamizi la kijiji itabaki kijijini |
| Wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji kufanya mikutano kila mwezi na kuwasilisha taarifa kwa Serikali ya Kijiji na kila baada ya miezi mitatu kwenye mkutano mkuu wa kijiji. | Asilimia2.5 ya mrabaha utokanao na mauzo ya mazao ya misitu kulipwa kwa serikali ya kijiji na inayobaki kulipwa kwa mmiliki wa shamba la miti |
| Kuzuia, kudhibiti na kuzima moto msituni kwa kushirikiana na uongozi wa shamba la miti | Kuingia msituni kuchuma mboga za majani, uyoga, kuchukua dawa bila kuathiri mti, kuokota mbegu, kamba, kukata nyasi kwa ajili ya malisho na kuezekea, kuni kavu na kuokota matunda. Pia kupita njia za miguu kutoka Kijiji kimoja hadi kingine, kuhudumia maeneo ya makaburi, kugema ulanzi, kufanya matambiko na kuchota maji kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira |
| Wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji kutoa Elimu ya uhifadhi kwa jamii | Kuingia msituni kwa shughuli za ufugaji Nyuki kwa kufuata utaratibu uliowekwa |
| Kutoa taarifa ya utekelezaji na ufuatiliaji kwa maandishi ya kila mwezi kwa mmiliki wa msitu | Kupata fursa ya kulima katika maeneo yaliyoruhusiwa msituni inapowezekana |
| Kuwa na vitalu vya miti na kupandaji kwenye mashamba yao. | Kuingia msituni kwa shuguli za uvuvi na uwindaji utafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni za sekta husika |
| Kushiriki katika kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira ndani na nje ya misitu katika vijiji husika. | Kutega maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na umwagiliaji kwa vibali |

| | |
|---|---|
| Kusoma mapato na matumizi ya mafao ya kila mwezi kwenye mikutano mikuu ya Vijiji na kutoa nakala kwa mmiliki wa msitu (kwa ajili ya utawala bora) | Kupata udongo wa juu (top soil) kwa ajili ya bustani ya miche ya miti |
| Kushiriki katika mikutano yote inayohusu usimamizi na uendeshaji wa shughuli za msitu | Fursa ya ajira katika shughuli mbalimbali za usimamizi wa msitu. |
| Kuhakikisha kuwa alama za mipaka ya misitu haziharibiwi wala kuhamishwa | |

6. Andaa rasimu ya Mpango wa Usimamizi wa msitu wa hifadhi wa kijiji kwa kushirikiana na Kamati ya Maliasili ya Kijiji kwa kuzingatia matokeo ya tathmini ya rasilimali ya msitu .

## HATUA YA TATU: KURASIMISHA NA KUHALALISHA

***Shughuli Muhimu ni Pamoja na***

1. Andaa rasimu ya mkataba/makubaliano ya usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji kwa kuzingatia rasimu ya mpango wa usimamizi na makubaliano ya mgawanyo wa majukumu ya usimamizi wa msitu na mafao. Kama wanavijiji wameridhia kusimamia msitu wa hifadhi kama eneo moja la usimamizi mkataba mmoja utaandaliwa na halmashauri zote za vijiji zitatia saini mkataba huo. Kama msitu umegawanywa kwenye Maeneo ya Usimamizi wa Msitu ya Kijiji, kila kijiji kitahitajika kusaini mkataba wake binafsi.

2. Tunga sheria ndogo za kijiji kwa kuzingatia kanuni zilizowekwa kwenye mpango wa usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji na mkataba wa usimamizi wa pamoja. Sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili ya Kijiji pamoja na mpango wa usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Misitu la Kijiji kuwasilishwa kwenye mkutano mkuu wa kijiji kwa idhini.




3. Wasilisha Rasimu ya Mpango wa usimamizi wa misitu na sheria ndogo kwa Mtendaji Mkuu wa TFS kupata maoni yake (Kwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa) na kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (Kwa Msitu wa Hifadhi wa Mamlaka ya Serikali za Mtaa).

4. Kamilisha na kutia saini Mkataba wa Usimamizi wa Pamoja na pande zote zinazoingia mkataba baada ya makubaliano baina ya Mkutano Mkuu wa Kijiji na Mmiliki wa msitu.

**Jedwali la mwongozo wa watia sahihi katika mikataba mbalimbali**

| Umiliki na usimamizi wa msitu | Wadau katika Makubaliano | Watia saini kwenye Mkataba |
|---|---|---|
| Msitu wa Hifadhi wa Taifa (Hifadhi ya Vyanzo vya maji na Hifadhi Asilia) | Wakala wa huduma za misitu na Jamii | Meneja wa Misitu wa Wilaya<br>Mwenyekiti wa Kijiji<br>Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya (Shahidi) |
| Msitu wa Hifadhi wa Taifa (Hifadhi Kwa Matumizi) | Wakala wa huduma za misitu na Jamii | Meneja wa Misitu wa Wilaya<br>Mwenyekiti wa Kijiji<br>Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya (Shahidi) |
| Msitu wa Hifadhi wa Mamlaka ya Mtaa | Halmashauri ya Wilaya na Jamii | Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya<br>Mwenyekiti wa Kijiji |

| | | |
|---|---|---|
| Msitu unaomilikiwa au kusimamiwa na Sekta binafsi (mf. Shamba la Chai, Msitu wa kupandwa) | Sekta binafsi na Jamii | Halmashauri ya Wilaya<br>Mkurugenzi wa Kampuni,<br>Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya<br>Mwenyekiti wa kijiji |

Nakala za Makubaliano/mkataba zipelekwe kwa:

- Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya na Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani
- Mtendaji Mkuu - TFS
- Mkuu wa Wilaya

5. Wasilisha sheria ndogo kwenye mkutano wa kijiji ili kuzipitisha: Baada ya kuhusisha mapendekezo yote toka kwa wadau wasilisha rasimu ya sheria ndogo katika mkutano mkuu wa kijiji ili kuzipitisha

## HATUA YA NNE: UTEKELEZAJI

**Shughuli Muhimu Ni Pamoja Na: –**

1. ***Kuifanya Kamati ya Maliasili ya Kijiji kuwa na ufanisi.*** Kama mwezeshaji, utahitaji kuwasaidia wajumbe wa Kamati waliochaguliwa kukutana kwa mara ya kwanza na kuwapa mafunzo juu ya masuala mbalimbali ya usimamizi wa msitu.

2. ***Kuanza ulinzi wa msitu.*** Shauri na saidia Kamati ya Maliasili ya Kijiji kuunda timu ya doria ili kuweka ulinzi wa mara kwa mara msituni

Ni wajibu wa Kamati kuhakikisha kwamba kila mwanakijiji anajua kanuni za matumizi ya msitu na adhabu zake. Kila mwanakijiji anapaswa kujua kuwa hapaswi kulipa faini au ada bila kupewa risiti sahihi.







3. ***Kuanza kutunza taarifa muhimu na kusaidia ufuatiliaji*.** Msaidie katibu wa kamati kununua, kutumia na kutunza Kitabu cha Stakabadhi, Kitabu cha Makosa na Faini, Kitabu cha Vibali, Kitabu cha Mapato na Matumizi, Kitabu cha Kumbukumbu, Kitabu cha Doria na Fomu ya taarifa ya robo mwaka

4. ***Kukabiliana na uvamizi wa msitu***. *Uvamizi wa mpaka* na *Makazi au kilimo ndani ya msitu*.

5. ***Anza na kazi zinazohitaji ukarabati wa haraka*** kama vile kupanda ili kurejesha miti kandokando ya eneo la chemichemi ambalo limeharibiwa na litakalofungwa kuzuia mifugo.
   Kuweka vizuizi kwenye njia za mifugo msituni zilizoamriwa kufungwa na/ au
   kupunguzwa, kushikiza maeneo yaliyochaguliwa kunyweshea mifugo ndani ya msitu na
   kujaza makorongo marefu.

6. ***Jukumu lako mwenyewe***. Wewe sasa ni mwezeshaji. Jaribu kutofanya kazi ya Kamati kwa ajili yake.Wahimize kujitegemea. Kila wakati Kamati inapofanya maamuzi na kuyatekeleza, inawafanya waone kuwa rahisi kuamua na kutekeleza suala la pili.

Wanakijiji wanapaswa kuhamasishwa kugharamia shughuli zao wenyewe za siku kwa siku kutokana na mapato yatokanayo na msitu wao. Kwa njia hii shughuli zao zitakuwa endelevu na kufikia lengo la kujitegemea.

## HATUA YA TANO: KUFANYA MAPITIO NA KUTANGAZA KWENYE GAZETI LA SERIKALI

**Shughuli Muhimu ni Pamoja na**

1. ***Pitia Mfumo wa Usimamizi*.** Hii hufanyika kwa ubora zaidi wakati usimamizi shirikishi wa msitu kwa pamojaumefanyika kwa takribani miaka 2-3 baada ya kusaini mkataba nautekelezaji kuanza kwa kutathmini shughuli za usimamizi na kutathmini athari ya usimamizi shirikishi kwa pamojajuu ya msitu

2. ***Rekebisha mfumo na Mpango wa Usimamizi wa Msitu*.** Mabadiliko lazima yawasilishwe kwenye Serikali ya Kijiji na Mkutano Mkuuwa Kijiji kwa idhini yao. Ni vema Mpango uliorekebishwa kusomwa wote kwa ukamilifu.




## HATUA YA SITA: KUPANUA HUDUMA KATIKA MAENEO MAPYA

Kabla ya kupanua kwenye misitu mipya na vijiji:

1. ***Tathmini hali ya misitu katika wilaya nzima*..**
2. ***Wianisha vipaumbele na kuandaa mpango wa Utekelezaji*.**

   - Orodha ya maeneo yote ya misitu katika wilaya, ukigawa katika Misitu ya Hifadhi ya Taifa, Msitu ya Hifadhi ya Serikali za Mitaa, vijiji vyenye uwezekano mkubwa wa kuanzisha Msitu wa Hifadhi wa Kijiji au Msitu wa Hifadhi wa Jamii na uwezekano wa kuanzisha Misitu Binafsi.
   - Kwa kila hoja, makisio ya ukubwa wake, aina ya misitu, hali na vitisho vikuu.
   - Vipaumbele kwa ajili yahatua
   - Ratiba ya upanuzi (kazi inayoweza kufanywa na Wilaya)

- Gharama za kupanua Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii

3. ***Anzisha mfumo rahisi wa kiutawala***. Je umeanzisha Daftari la kusajili Mikataba ya usimamizi wa pamoja? Je, una jalada kwa ajili ya kila Mkataba wa usimamizi wa pamoja? Je, unatunza kumbukumbu ya ziara zako zote?

4. ***Anzisha mfumo rahisi wa kusaidia.*** Jinsi vijiji vinavyoendelea kushiriki ndivyo unavyohitaji kuwasaidia.

# SANDUKU LA MSAADA LA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU JAMII

**Yaliyomo**


**I MIFANO YA ZANA ZA KUTATHMINI MSITU**

1. Orodha ya matumizi yanayotarajiwa kutoka msituni
2. Solo ya matumizi ya msitu
3. Mfano wa fomu A iliyojazwa ya tathmini ya msitu
4. Mfano wa fomu B iliyojazwa ya tathmini ya msitu
5. Mfano wa fomu C iliyojazwa ya tathmini ya msitu

**II MIFANO YA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU**

A Muhtasari wa kumbukumbu muhimu za kuwekwa katika ngazi ya kijiji

1. Mfano wa ukurasa wa daftari la kibali naleseni
2. Mfano wa ukurasa wa daftari la uhalifu nafaini
3. Mfano wa kurasa za daftari la mapato na matumizi
4. Mfano wa ukurasa wa daftari la doria
5. Mfano wa ukurasa wa taarifa ya robo mwakaya utekelezaji wa usimamizi wa msitu

B Mfano wa ukurasa wa rejesta ya Wilaya Misitu ya Vijiji

**III MFANO WA MIUNDO**

1. Makubaliano/mkataba wa usimamizi wa msitu kwa Pamoja
2. Mpango wa usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji
3. Sheria ndogo za Vijiji za Usimamizi Shirikishi wa Msitu kwa Pamoja

## III MFANO WA MIUNDO

## 1 MFANO WA MUUNDO WA MAKUBALIANO YA USIMAMIZI WA PAMOJA

Mkataba wa Usimamizi wa Pamoja kati ya Mtendaji Mkuu - TFS / Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya,Wilaya X na kijiji X, wilayaX, kwa mujibu wa Eneo la Usimamizi wa Msitu la Kijiji (EUMK) X katika Msitu wa Hifadhi X.

| | |
|---|---|
| Sehemu ya 1: | Inaelezea EUMK liliokusudiwa, mahali lilipo na mipaka yake |
| Sehemu ya 2: | Sehemu hii inaorodhesha mambo yaliyo chini ya makubaliano hayo. |
| Sehemu ya 3: | Sehemu hii inaorodhesha malengo ya Mkataba. |
| Sehemu ya 4: | Sehemu hii inabainisha wadau katika mkataba |
| Sehemu ya 5: | Sehemu hii inamtambua meneja wa EUMK na kuainisha majukumu yake. |
| Sehemu ya 6: | Sehemu hii inaelezea majukumu ya usimamizi wa msitu kwa Kamati ya Maliasili ya Kijiji (KMaK) |
| Sehemu ya 7: | Sehemu hii inabainisha kanuni za upatikanaji na matumizi ya msitu kama zinavyofafanuliwa kwenye Mpango wa Usimamizi wa Msitu na sheria ndogo. Pia inabainisha mgawanyo wa mafao yatokanayo na usimamizi wa msitu. |
| Sehemu ya 8: | Sehemu hii inabainisha ni nani mwenye haki ya ya kutumia EUMK kama inavyobainishwa katika mpango wa usimamizi na sheria ndogo |
| Sehemu ya 9: | Sehemu hii inaelezea kuwa mapato kutoka vyanzo mbalimbali kutunzwa kwenye akaunti ya KMaK na kutumiwa kwa mujibu wa mpango wa usimamizi na umuhimu wa kutunza kumbukumbu na wajibu wa Halmashauri ya Wilaya/ mtu aliyeteuliwa na Wakala wa Huduma za Misitu kukagua mahesabu. |
| Sehemu ya 10: | Sehemu hii inaweka utaratibu wa kusuluhisha migogoro miongoni mwa wadau |
| Sehemu ya 11: | Sehemu hii inabainisha watia saini kwenye mkataba, muda wa mkataba na kama muda wa mkataba unaweza kuongezwa |
| Sehemu ya 12: | Viambatisho ambazo ni sehemu ya mkataba huu ni pamoja na sheria ndogo za kijiji za usimamizi wa msitu na mpango wa usimamizi wa EUMK |
| Sehemu ya 13: | Sehemu hii inaweka utaratibu wa kurekebisha mkataba |
| Sehemu ya 14: | Sehemu hii inabainisha kifungu katika mpango wa usimamizi wa msitu kitakachotumika kutoa adhabu. |
| Saini: | Sehemu hii inabainisha watia saini katika mkataba huu na mashahidi kwa makubalianao; |

## 2 MFANO WA MUUNDO WA MPANGO WA USIMAMIZI WA ENEO LA USIMAMIZI WA MSITU LA KIJIJI

Sehemu ya 1: Inahusu maelezo ya jumla kuhusu Mpango

Sehemu ya 2: Inahusu maelezo ya msitu wenyewe, matumizi ya msitu na jamii inayohusika katika kusimamia msitu.

Sehemu ya 3: Inaorodhesha madhumuni ya kuuweka msitu wote chini ya usimamizi uliojikita kwa jamii.

Sehemu ya 4: Inaainisha nani atakuwa Meneja - kwa kawaida ni Kamati ya Usimamizi ya Msitu wa Kijiji (Kamati ya Maliasili ya Kijiji).

Sehemu ya 5: Inaorodhesha kumbukumbu zote ambazo zitawekwa kuhusiana na usimamizi wa msitu.

Sehemu ya 6: Inaeleza kuhusu usimamizi wa fedha kwa uwazi ili kuzuia USMP kukwama kwa sababu ya usimamizi mbaya wa fedha.

Sehemu ya 7: Inaelezea mpaka wa pembeni wa msitu, mipaka ya maeneo ya usimamizi wa msitu ya kila kijiji, Kanda za Usimamizi za Msitu na Mipakaya Maeneo Maalum.

Sehemu ya 8: Inaelezea kuhusu ulinzi wa msitu ambayo ndio shughuli kubwa katikaUSMP. Inazungumzia watu watakaofanya doria, shughuli zao, uwajibikaji na tuzo kwa kukamata wahalifu au mafanikio katika kulinda msitu.

Sehemu ya 9: Inaelezea jinsi msitu utakavyovunwa na kutumika

Sehemu ya 10: Inaweka kanuni za kufikika kwa msitu, matumizi na kanuni zingine za kusimamia msitu.

Sehemu ya 11: Inaweka taratibu za kushughulikia makosa viwango vya faini kwa kila kosa, faini ya uwajibikaji, adhabu zingine ambazo zinaweza kutolewa na jinsi ya kushughulika mtu aliyeshindwa kukiri kosa au kulipa faini.

Sehemu ya 12: Inaorodhesha shughuli zozote zilizopangwa kwa ajili ya kukarabati msitu au

Sehemu ya 13: Inaweka utaratibu wa kutoa taarifa, kufuatilia na kutathmini

Sehemu ya 14: Inaweka utaratibu wa kutatua migogoro baina na kati ya vijiji.

Sehemu ya 15: Inaweka mpangokazi wa mwaka na kuweka malengo na muda kwa kila tendo.

.

## 3 MFANO WA MUUNDO WA SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MSITU KWA PAMOJA

Sehemu ya 1: Inataja jina/kichwa cha Habari cha Sheria Ndogo

Sehemu ya 2: Inaonesha somo na Lengo la Sheria ndogo, jina la msitu na kuelezea taarifa za msitu na nia ya Sheria hizo.

Sehemu ya 3: Inamtambua Meneja [Kamati ya Maliasili ya Kijiji] kipindi cha kuwa madarakani na jinsi kamati mpya itakavyochaguliwa na inaweka wazi majukumu na mamlaka yake.

Sehemu ya 4: Inaelezea shughuli za ulinzi wa msitu na inaweka wazi kanuni za jinsi ya kusimamia msitu.

Sehemu ya 5: Inaweka wazi kila kanuni au ‘sheria’ ya kuingia na kutumia msitu.

Sehemu ya 6: Inaweka adhabu stahiki kwa kila kanuni itakayovunjwa.

Sehemu ya 7: Inaweka taratibu za kukamata wahalifu na kutozwa faini, jinsi ya ulipaji faini na kupewa stakabadhi.

Sehemu ya 8: Inaweka wazi jinsi mapato yatakayotokana na faini na ada yatakavyotunzwa na kutumika.

Sehemu ya 9: Inaeleza marekebisho, ambayo si kinyume na lengo la Sheria ndogo, yanaweza kubadilishwa. Nakala ya taarifa ya mabadiliko lazima iwasilishwe Halmashauri ya Wilaya.

Sehemu ya 10: Inaeleza tarehe ambayo Sheria ndogo itaanza kutumika.

# Kampeni ya Mama Misitu

Mama Misitu ni Kampeni ya mawasiliano inayolenga kuboresha utawala wa Misitu Tanzania, na kukuza matumizi endelevu ya mazao ya Misitu ili watu wa Tanzania wanufaike zaidi na rasilimali za Misitu. Kampeni ya Mama Misitu imebeba dhamira na maono ya kuhifadhi, kulinda na kuhamasisha matumizi endelevu ya Misitu. Kampeni ya Mama Misitu inatekelezwa na kikundi kazi cha misitu Tanzania na kuratibiwa na Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF).

LAWYERS ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)

JOURNALISTS ENVIRONMENTAL ASSOCIATION OF TANZANIA

TRAFFIC the wildlife trade monitoring network

Femina HIP

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA • MJUMITA •

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Mpingo Conservation & Development Initiative

policy forum

Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

# Tumerithi




# Tuwarithishe

Kampeni ya Mama Misitu, Namba 27 Mtaa wa Sangara - Mikocheni, Dar es Salaam. I **Tovuti:** www.mamamisitu.com I **Barua pepe:** info@mamamisitu.com I **Simu:** +255 758828398 I **Facebook:** www.facebook.com/mamamisitu I **Twitter:** www.twitter.com/mamamisitu

Uandaaji na uchapishaji wa mwongozo huu pamoja na Kampeni ya Mama Misitu vimefadhiliwa na Serikali ya Ufini.

FORMIN.FINLAND.FI

MINISTRY FOR FOREIGN AFFAIRS OF FINLAND